SautiElimu

hakielimu

Toleo la 1
2002

ISSN 0856 8588



Je, sauti yako inasikika?

Kutoka kwa Mhariri

Na Rakesh Rajani, Mkurugenzi Mtendaji, HakiElimu

Wote tunajali elimu. Licha ya hali ngumu, mamilioni ya wanafunzi bado wanahangaika kujifunza na kufurahia maisha ya shule. Zaidi ya walimu 100,000 bado wanajitahidi kufundisha licha ya mishahara midogo na hali duni ya mazingira ya kazi. Na karibu kila mmoja wetu ama ni mzazi, kaka au dada wa mtoto fulani anayejitahidi kupata elimu.

Lakini je, sauti zetu zinasikika katika elimu? Je, sauti yako inasikika?

Mara nyingi, shule zina uongozi unaotoa mwanya mdogo kwa watu wa kawaida kuuliza maswali, kutathmini na hata kutoa maoni kuhusu jinsi ya kuboresha elimu. Maagizo hutoka ngazi za juu, bila kutaka ushauri wa watu wa chini ambao ndio huathirika zaidi na maamuzi hayo. Watu wanapokuwa na maoni yao mara nyingi hawapati pakuyapeleka. Matokeo yake elimu inakosa mchango wa jamii katika kuiboresha.

Hali hii haitakiwi kuendelea. Mipango ya Serikali ya Kurekebisha Serikali za Mitaa na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) inatambua umuhimu wa kukuza ushiriki wa jamii katika elimu na kuimarisha uwazi na uwajibikaji. Pia inasisitiza umuhimu wa kutoa fursa kwa watu wa kawaida hasa wale ambao mara nyingi sauti zao hazisikiki.

Kila mtu aielewe bajeti ya shule na jinsi fedha zake zinavyotumika. Kila mtu awe na uhakika kwamba kamati ya shule itasikiliza kero zake. Kila mtu apate nyaraka za msingi za sera za elimu. Kwa hiyo kuzipata na kuzijadili taarifa ni muhimu kwa utawala bora.

Jarida hili, ambalo litatolewa mara tatu kwa mwaka, ni nafasi yako ya kutoa maoni na kujifunza kutoka kwa wengine. Hii ni sauti yako! Ongea na rafiki yako kuhusu wazo la jarida hili! Waulize viongozi wako kuhusu masuala yaliyojadiliwa humu. Tueleze mawazo yako! Pia, tafadhali tupe mawazo yako kuhusu jarida hili, likoje? Je, linaongelea mambo unayotaka kuyafahamu?



Walimu Wahusishwe katika Uongozi wa Shule!

Na Ezekiel Oluoch, Chama cha Walimu Tanzania (CWT)

Ili kuboresha elimu, mwalimu hana budi kuhusishwa katika uongozi. Uwakilishi wa walimu kwenye kamati za shule ni muhimu kwani kamati zinatoa maamuzi kuhusu maendeleo ya shule.

Ni muhimu wawakilishi wa walimu wachaguliwe na walimu wenyewe bila ya shinikizo kutoka utawala wa juu. Wanaochaguliwa kuwakilisha kwa njia hii huaminiwa na walimu wenzao kuwa wana uwezo wa kuwakilisha matatizo ya wenzao.

Uwakilishi wa walimu pia unakuwa na umuhimu wake pale ambapo kero zinazowakatisha tamaa hujadiliwa na kupatiwa ufumbuzi. Katika suala la kuboresha taaluma, wenye nafasi ya kuchangia kwa ufasaha mbinu mbalimbali ni walimu wenyewe wenye uzoefu katika utendaji kazi.

kwa ajili ya ujenzi wa madarasa na uendeshaji shule. Kiasi cha fedha kinachotolewa na matumizi yake yawe wazi ili kila mwalimu afahamu ni vipi fedha za shule yake zinavyotumika.

Ni tabia ya binadamu kufurahia anapotekeleza maamuzi ambayo yeye pia alipewa nafasi ya kuchangia mawazo yake. Hivyo basi, mwalimu awe na nafasi ya kubuni mbinu za ufundishaji kulingana na mazingira ya mahali alipo.

Mwalimu ni kiongozi katika jamii na ni mfano bora wa kuigwa na jumuiya inayomzunguka. Hata kama anakosea, ni bora apewe nafasi ya kujitetea katika kamati inayomjadili ili aridhike kwamba anatendewa haki.

Ni hatari kwa jumuiya yeyote ile kupanga mikakati ya elimu na kumweka kando mtendaji wake mkuu ambaye ni mwalimu. Hiyo ni sawa na kujadili upatikanaji wa umeme unaotokana na maji bila kuwa na mvua. Bila kumhusisha mwalimu katika mipango ya maendeleo, hapatakuwa na shule bora.



Vilevile walimu wanahitaji kuwa na uwakilishi katika vikao vya kujadili mapato na matumizi ya fedha zinazotolewa

Je, unajua shule nzuri? Mwalimu mzuri?

Tuarifu na ujishindie zawadi nono!

Kuanzia toleo lijalo la SautiElimu tutatoa maelezo ya Shule Nzuri na/au Mwalimu Mzuri. Tunahitaji msaada wako wa kutafuta shule bora na mwalimu mzuri nchini Tanzania. Shule nzuri ni ipi? Mwalimu mzuri ni yupi?

Tuandikie Haki Elimu, SLP 79401 Dar es Salaam

Yafuatayo ni baadhi ya mawazo machache yatakayokusaidia!

Walimu wazuri…..


- wanathamini kazi zao
- wanaipenda kazi yao
- wako tayari kujifunza
- wanawachochea wanafunzi wafikiri
- Wanawezesha wanafunzi kujiamini
- Wanawafanya wanafunzi wapende kusoma
- wanashirikiana kwa ukamilifu na jumuiya pana ya shule
- wanajali

Shule nzuri…..

- zina viongozi wanaowajibika na wanaoshiriki
- wanahimiza ushiriki wa watu wote katika jumuiya
- wako tayari kupokea maoni ya wazazi
- wanawashirikisha wanafunzi katika kutoa maamuzi
- wanatoa elimu bora inayowafunza wanafunzi kufikiri na kuwa wabunifu kwa ukamilifu
- hawachapi wala kuwadhalilisha na kuwaonea wanafunzi kama njia ya kuwaadabisha
- wanajenga mazingira mazuri ya ukarimu na upendo
- wanahamasisha wengine kuthamini elimu

Tutumie mapendekezo yako ya shule au mwalimu bora nchini Tanzania. Unapotuandikia, tafadhali tuarifu:

- Jina la shule au mwalimu
- Namna tutakavyowasiliana nao, kwa mfano; anwani, simu, iwapo wanayo
- Kwa nini unampendekeza mwalimu au shule nzuri



Iwapo shule utakayoipendekeza au Mwalimu utakayempendekeza ataandikwa kwenye machapisho, utapata fulana ya HakiElimu. Na iwapo utapendekezwa kuwa mwalimu mzuri au shule yako kuwa bora pia tutakupa zawadi!

Shukrani ziwaendee Ecoliers du Monde, Mwanza, asasi zisizo za kiserikali (NGO) na watu binafsi waliotoa mawazo yao kupitia barua pepe wakati wa mwezi Mei 2002.



Wanafunzi wapo katika Utawala wa shule?

Na Zitto Kabwe, Mtandao wa Wanafunzi Tanzania (TSNP)

Wanafunzi wana haki ya kushiriki katika uendeshaji wa shule kuanzia uongozi wa wanafunzi hadi uwakilishi kwenye kamati za shule.

Kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM), Halmashauri ya Wanafunzi itawachagua wawakilishi wawili watakaoingia katika kamati ya shule. Ushirikishwaji wa wanafunzi utafanywa katika njia inayoakisi kanuni za msingi za uwakilishi wa kidemokrasia, usawa na jinsia.

Kila shule inatakiwa kuwa na uongozi wa wanafunzi uliochaguliwa na wanafunzi wenyewe. Hata hivyo, utafiti unaonyesha kuwa shule chache zina viongozi wanafunzi waliochaguliwa na wenzao kidemokrasia. Viongozi wa shule kadhaa wamekuwa wakiteuliwa na baadhi ya walimu. Je, viongozi wanaoteuliwa na walimu watasimamia maslahi ya nani? Je, hii ndiyo namna ya kufundisha demokrasia?



Viongozi wanafunzi kawaida hufanya kazi zifuatazo:

- kuandika majina ya wafanya fujo ili waadhibiwe na mwalimu,
- kusimamia wanafunzi katika kufanya shughuli za shule kama vile usafi wa mazingira
- kupokea maamuzi kutoka kwa walimu na kuyapeleka kwa wanafunzi wenzao kwa utekelezaji, bila majadiliano

Je, kazi hizo zinampa mwanafunzi uwezo wa kupanua mawazo yake na kuwa mbunifu? Kwa mfumo huo, viongozi wa wanafunzi wanazoea kupokea amri tu na kusimamia wenzao. Hali hiyo inawajenga kuwa viongozi wanyapara wasio na uhusiano bora na wenzao.

Katika uongozi wa shule mara nyingi, kaka mkuu ndiye mkubwa na dada mkuu huwa msaidizi wake. Huu ni ubaguzi wa kijinsia! Mtoto anajifunza tangu awali kwamba mwanaume ana uwezo mkubwa ikilinganishwa na mwanamke.

Lengo kuu la elimu ni kumwezesha mwanafunzi kukabili maisha ya baadaye na kuiendeleza jamii yake. Tutaweza tu kufikia lengo hili iwapo tutampa mtoto nafasi ya:

- kujieleza na kutoa maoni yake katika mambo yanayomhusu
- kuchagua viongozi wake ili kutetea maslahi yake bila woga
- kushiriki katika kamati za shule
- kuondoa ubaguzi wa kijinsia usio na maana (mfumo dume) katika nyanja ya uongozi wa wanafunzi kuanzia darasani
- kuwa na mfumo wa viongozi kuendelea kuwasiliana na wanafunzi wenzao kila wakati


Wezesha wanafunzi kujieleza! Wape nafasi ya kushiriki katika uongozi wa elimu!

Ukurasa wa 1

SautiElimu

hakielimu

Toleo la I
2002
ISSN 0856 8588



Matukio katika Elimu -Mkutano wa kilele wa G8

Baadhi yenu mmewahi kuona kadi za posta zilizosambazwa wakati wa Wiki ya Elimu kwa Wote, mwezi Aprili 2002. Kadi hizi za posta ziliwahimiza wahisani kuelekeza juhudi zao katika Elimu kwa Wote na zilipelekwa kwa Waziri wa Elimu na Utamaduni nchini Tanzania na kwa Waziri Mkuu wa Canada, ambaye pia ni mwenyekiti wa mkutano wa kilele wa G8.

G8 ni nini?

Mkutano wa kilele wa G8 hufanyika kila mwaka ili kusaidia kupata ufumbuzi au majibu ya masuala ya msingi duniani. Mkutano wa mwaka huu ulifanyika Kananaskis nchini Canada tarehe 26-27 June, 2002. Wajumbe wanane wa mkutano huo ni Ufaransa, Marekani, Uingereza, Ujerumani, Japani, Italia, Canada na Urusi. ("G" inasimama badala ya "Group" na "8" badala ya idadi ya nchi wanachama)

Je, mkutano ulijadili nini?

Mkutano huu umezingatia mambo matatu muhimu: ukuaji wa uchumi duniani, maendeleo ya bara la Afrika na kupambana na ugaidi. Aidha walijadili maendeleo ya kukuza elimu ya msingi kwa wote (UPE).

Je, viongozi wa G8 wameahidi nini?

Viongozi wa G8 walitambua umuhimu wa elimu, hasa barani Afrika. Rais George Bush wa Marekani amekubali kuongeza fedha za serikali kwa ajili ya elimu barani Afrika kwa ongezeko la dola za kimarekani milioni 200. Benki ya Dunia imetangaza mpango wa utekelezaji wa "kupeleka haraka" msaada wa elimu kwa nchi 17. Tanzania ni nchi mojawapo kati ya zilizochaguliwa kupata msaada. Wakati hizi ni habari nzuri, kiwango cha msaada ni kidogo ukilinganisha na mahitaji na kiasi cha fedha kinachotumika kwa masuala mangine.

Je, Tanzania itafaidika?

Baadhi ya fedha zinaweza kusaidia Serikali ya Tanzania kuziba pengo la bajeti lililopo hivi sasa katika kugharamia Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi (MMEM). Muhimu zaidi, itaweza kutoa fedha zaidi kwa maeneo yanayohitaji msisitizo zaidi, kama vile ubora wa elimu inayotolewa.

Hata hivyo, yote haya yanategemea namna Serikali itakavyopanga bajeti yake, na namna itakavyohakikisha kuwa fedha zinafika hadi shuleni. Ndio maana Serikali za nchi za G8 na Tanzania zinahitaji kusikia kutoka kwako kuhusu vipaumbele vyako muhimu katika elimu!



Kuwa Rafiki wa Elimu sasa!

Nini madhumuni ya marafiki wa elimu?

Mtandao wa Marafiki wa Elimu una madhumuni ya kuongeza ushiriki katika elimu kwa Wananchi wote nchini Tanzania. Mtandao huo utatoa taarifa halisi kwa watu wanaojali elimu nchini Tanzania. Utawasaidia kutoa maoni yao na kero katika vyombo vinavyohusika. Pia mtandao utawaunganisha marafiki ili waweze kuleta mabadiliko katika shule na kuziwezesha kutoa elimu bora kwa watu wote. Baada ya muda wazo ni kwamba mtandao wa marafiki utasaidia kufuatilia na kutoa mwelekeo wa elimu nchini Tanzania.

Je, utafaidika nini kwa kuwa rafiki?

Kuwa Rafiki wa Elimu kutakupa nafasi au fursa kuelewa nini kinachoendelea kuhusu masuala ya elimu. Unaweza kutuletea maswali yako na tutajitahidi kukujibu, nakukuunganisha na watu wenye majibu. Iwapo unataka usikike , tutajitahidi kufikisha mawazo na kero zako kwa viongozi wahusika.

Mtandao wa marafiki pia utakupa fursa ya kuchangia au kubadilishana mawazo na uzoefu wa watu wengine wanaojali elimu. Tutakuza fursa zako za kujifunza kutoka kwa wenzako na kushirikiana ili kuhakikisha kwamba kila mtoto anafurahia elimu ya msingi iliyo bora.

Utapata nakala za kijarida chetu cha "SautiElimu" mara tatu kwa mwaka, kalenda yetu ya mwaka na machapisho mengine. Hii itakusaidia kuelewa maswala ya kila siku kuhusu elimu na shughuli za Marafiki wa Elimu nchini Tanzania.

Nani anaweza kuwa rafiki ?

Mtu yeyote na kila mtu anaweza kuwa Rafiki wa Elimu! Hakuna masharti. Unaweza kuwa mzee au kijana, mwanamke au mwanaume, shuleni au nje ya shule. Licha ya watu binafsi, pia tunakaribisha maombi kutoka kwa vikundi na mashirika.

Nitakuwaje rafiki? Nitajiunga lini?



Uanachama ni bure! Ili kujiunga, tafadhali tuandikie jina, umri, jinsi, anwani kamili na maelezo mafupi kuhusu kwa nini unajali elimu. Tunatarajia kwa hamu kupata maoni kutoka kwako!

Tunakamilisha maandalizi ya kuanza mtandao wa marafiki na unaweza kuomba kujiunga, na tutakujibu kuanzia mwezi September 2002. Wasiliana nasi kwa anwani ya:

Marafiki wa Elimu
HakiElimu
SLP 79401
Dar es Salaam

Barua Pepe:
rafiki@hakielimu.org

HakiElimu ni shirika la hiari linalolenga kufikia usawa, ubora, haki za binadamu na demokrasia katika elimu kwa kuwezesha jamii kubadili shule na mfumo wa uundaji wa sera za elimu, kuimarisha ubunifu wa uendeshaji wa mijadala na midahalo ya umma, kufanya utafiti yakinifu, wenye kuhoji, wenye kuchambua, kutetea na kushirikisha wadau ili kuendeleza manufaa ya pamoja na kuzingatia haki za jamii.

Shukurani kwa Shule za Msingi za Getasamo, Nyamoko (Serengeti) na Busagami (Ukerewe), Jumuiya ya Kimara-Barafu (Dar es Salaam) na Richard Evans wa Concern.

Unaruhusiwa kunakili sehemu yeyote ya jarida hili kwa minajili isiyo ya kibiashara. Unachotakiwa kufanya ni kunukuu chanzo cha sehemu iliyonakiliwa na kutuma nakala kwa HakiElimu.

ISBN 998- 8943-1-3

© HakiElimu, 2002

Mhariri: Rakesh Rajani
Timu ya SautiElimu: Lilian Kallaghe, Kathy Relleen na Godfrey Telli
Kutafsiri: Albert Mazzuki, Lilian Kallaghe na Godfrey Telli
Mchoraji: Marco Tibasima

Tuandikie!

HakiElimu, SautiElimu
SLP 79401
Dar es Salaam
Simu: 022 2151852 / 3
Faksi: 022 2152449
Baruapepe: info@hakielimu.org
Tovuti: www.hakielimu.org



Ukurasa wa 2

Barua kwa SautiElimu



Mhariri SautiElimu, Mimi ni mjumbe wa Kamati ya shule. Mara kwa mara tunapokuwa na vikao vya kamati, mwenyekiti wetu hatupi nafasi ya kuzungumza. Mwenyekiti anakuwa mkali tunapouliza maswali na kudai kuwa anatakiwa kutupa tu taarifa na kwamba kila kitu ameshapanga kwa kushirikiana na mwalimu mkuu. Je, huu ndio utaratibu?

Mjumbe Mkereketwa
Tabora

Mjumbe mkereketwa, Ahsante kwa barua yako. Mwenyekiti wa Kamati ya shule yako hafuati utaratibu. Kamati inatakiwa kufanya kazi kwa uwazi na kutoa maamuzi kidemokrasia. Wanakamati wote wana haki ya kufahamu na kushiriki katika kutoa maamuzi yanayoleta maendeleo ya shule. Wasiliana na uongozi wa elimu katika tarafa au wilaya yako upate miongozo ya jinsi kamati za shule zinavyopaswa kuendeshwa.

Tunakushauri kutoa malalamiko yako kwenye kikao cha kamati ya shule baada ya kujadiliana na wanakamati wenye mtizamo kama wako. Ukikwama wasiliana na uongozi wa elimu wa mtaa/kijiji kwa ufafanuzi zaidi.

•••

Mhariri SautiElimu, Hivi karibuni serikali ilifuta ada za kuandikisha watoto shule na michango mbalimbali. Je, sisi kama wazazi kuna haja ya kutoa michango mingine kama vile ya mitihani na shughuli nyingine za maendeleo?

Wazazi
Mwanza

Ni kweli kwamba serikali imefuta ada. Hakuna tena mtoto atakayefukuzwa shule kwa kukosa ada na michango mingine. Hakuna tena wazazi kulazimishwa kutoa fedha kwa ajili ya michango mbalimbali ya shule. Lakini pia jamii inawajibu wa kuhakikisha kwamba elimu inaboreshwa kwa ajili ya watoto wote. Hivyo michango ya hiari hasa ya nguvukazi bado inatarajiwa kutoka kwa jamii ili kuleta maendeleo na ufanisi wa elimu.

•••

Mhariri SautiElimu, Tumesoma kupitia vyombo vya habari kwamba kamati za shule zina jukumu la kupanga na kutoa tathmini ya mapato na matumizi ya fedha za shule. Je, ni utaratibu gani unaotumika kutoa taarifa? Je, Kamati za shule zinawajibika kwa nani? Wanakijiji wanaweza kuziwajibisha kamati kama zitakwenda kinyume na utaratibu?

Wanakijiji
Mwalusembe

Utaratibu wa kutoa taarifa kuhusu mapato na matumizi ni wa kamati za shule. Taarifa zote za mapato na matumizi zinatakiwa kuwa wazi kwa wadau wote wa elimu. Hawa ni pamoja na wazazi, wanafunzi, walimu, viongozi wa serikali za mtaa/kijiji. Kamati zinawajibika kwa wadau hao. Hivyo basi, kama utendaji wa kamati utakuwa na upungufu basi wadau wana haki ya kuwawajibisha wanakamati.

•••

Mhariri SautiElimu, Tumesikia kwamba serikali imetenga shilingi 9,000/- kwa kila mwanafunzi, kwa mwaka. Je, fedha hizo ni kwa ajili ya matumizi yapi? Tunaomba ufafanuzi kwani tunahofu kwamba fedha hizo huenda zisitumike kwa matumizi yaliyokusudiwa.

Wanafunzi
Mtwara

Kwa mujibu wa MMEM, ni kweli kwamba serikali imetenga shilingi 9,000/- kwa kila mwanafunzi kwa mwaka. Fedha hizo ni kwa ajili ya kuinua ubora wa elimu shuleni. Kati ya fedha hizo, shilingi 3,600/- zitakwenda kwenye uongozi wa elimu wa wilaya kwa ajili ya kununulia vitabu vya shule. Salio, yaani shilingi 5,400/- zitakwenda moja kwa moja shuleni kuboresha elimu. Ulizeni kwa viongozi wa shule ili kuhakikisha mnapata fedha hizo.

•••

Mimi ni mwanafunzi wa darasa la saba shule ya msingi Umoja. Ningependa kufahamishwa kama ni kweli kwamba muundo wa kamati za shule unatoa nafasi kwa wanafunzi kuwa wajumbe. Kama ni kweli, kwa nini basi kamati yetu ya shule haijumuishi wanafunzi?

Mwanafunzi
Umoja Shule ya Msingi

Ahsante kwa swali lako. Kwa mujibu wa MMEM, utaratibu wa ushiriki wa wanafunzi katika utawala wa shule uko wazi. Ni kwamba wanafunzi wawili watatoka katika kila mkondo (mvulana 1, msichana 1) watachaguliwa na vijana wa rika lao kuwa wajumbe wa baraza la wanafunzi. Baraza la wanafunzi litaundwa na mkutano wa wakilishi wote wa wanafunzi.

Uongozi wa baraza la wanafunzi uliochaguliwa kidemokrasia utawajumuisha wawakilishi wawili katika kamati ya shule. Wawakilishi wa wanafunzi katika kamati ya shule watapokea maagizo yao kutoka katika baraza la wanafunzi na kutoa taarifa kwa baraza hilo hilo.

Tuandikie!

Barua kwa SautiElimu,
HakiElimu SLP 79401 Dar es Salaam
Barua Pepe: sautielimu@hakielimu.org

Vyanzo vya Taarifa

Machapisho ya HakiElimu

Machapisho yafuatayo yanapatikana bila malipo yoyote:
Kijarida cha 'HakiElimu ni nini?'
Kijitabu cha 'Hii Ndio Elimu?'
Mlolongo wa mabango yenye ujumbe unaohusu Utawala wa Elimu na Elimu Bora.

Watu binafsi na mashirika wanaweza kuomba nakala moja ya SautiElimu bure! Kama unahitaji kujiorodhesha kwa ajili ya kupata nakala zijazo za jarida hili au kupata nakala zaidi ya moja, tafadhali tujulishe kupitia anwani hii:

HakiElimu
Idara ya Ushiriki wa Umma,
SLP Box 79401
Dar es Salaam
Barua Pepe: pubs@hakielimu.org
Tovuti: www.hakielimu.org

